/TANGAZO LA SERIKALI NA. 244 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MAGOROFANI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Magorofani ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa nakuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe.

*Tangazo la Serikali Na. 244 (Linaendelea.)*

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A1 yenye majira - nukta 377813MS, 9615175KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini- Mashariki katika uelekeo wa $84^0$ kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba A2 yenye majira - nukta 377561MS, 9615479KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $147^0$ kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba A3 yenye majira - nukta 3777188MS, 9615685KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa $165^0$ kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba A4 yenye majira - nukta 376954MS, 9615691KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $113^0$ kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba A5 yenye majira - nukta 376836MS, 9615436KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $106^0$ kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba A6 yenye majira – nukta 377234MS, 9615037KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $106^0$ kwa umbali wa kilomita 0.1 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba A7 yenye majira ya nukta 377324MS, 9615130KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $83^0$ kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba A8 yenye majira - nukta 377566MS, 9614937KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa $96^0$ kwa umbali wa kilomita 0.1 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba A9 yenye majira - nukta 377659MS, 9615062KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa $87^0$ kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi ulipoanzia''

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*